
# Prophet Muhammad

Book 1 of 5:

# Muhammad Mtume wa Allah - Kidokezo kifupi cha wasifa




## Sayyid Muhammad Rizvi



Al-Ma'arif Publications

**Mfululizo wa vitabu juu ya Mtume Muhammad**

**Kitabu cha 1 ya 5**

# MUHAMMAD
## MTUME WA ALLAH
### *Kidokezo kifupi cha wasifa*


**Kuzaliwa mpaka kuanza kwa Wahyi . . . 1**
**Kuanza kwa Ujumbe . . . 2**
**Kuhamia Medina . . . 5**
**Kuanzisha Jamii ya Kiislamu . . . 6**
**Mapambano katika Medani za vita . . . 7**
(a) Vita vya Badr . . . 7
(b) Vita vya Uhud . . . 8
(c) Vita vya Khandaq (*Ahzab*) . . . 9
(d) Vita vya Bani Qurazah . . . 9
(e) Vita vya Bani Mustalaq . . . 9
(f) Vita vya Khaybar . . . 9
**Mkataba wa Hadaybiyah na kuanguka kwa Makkah . 10**
**Hijjah ya Mwisho na Kifo . . . 11**
**Heshima ya La Martine kwa Mtume . . . 12**



***Sayyid Muhammad Rizvi***


Kimetarjumiwa na:
**Ramadhani Kanju Shemahimbo**

Ilichapishwa mara ya kwanza na:
Al-Itrah Foundation

Toleo la Kwanza (Dar es Salaam) 2008
**Toleo la Pili (Toronto) 2020**

ISBN : 978-0-920675-56-4

© 2020 Haki za kunakili imehifadhiwa.

Chapisho hili linaweza kusambazwa kwa kuchapishwa au kwa njia ya kielektroniki, hata hivyo haipaswi kubadilishwa kabisa, kwa sehemu au nzima, bila idhini ya maandishi ya mchapishaji.

Kimetolewa na

**Al-Maʿārif Publications**
Toronto, Canada

www.al-m.ca | publications@al-m.ca | (+1-416) 624-7861

Kimepangwa na kuendeleza kwenye mfumo wa kigitali na
www.shia-maktab.info

# MUHAMMAD MTUME WA ALLAH

## NENO LA MCHAPISHAJI
## (*wa toleo la kwanza la Kiswahili*)

Kijitabu ulicho nacho mikononi mwako ni tarjuma ya Kiswahili kutoka Kiingereza.

Maandishi ya asili ya Kiingereza yaliandikwa na mwanachuoni mashuhuri wa Kiislamu Sayyid Muhammad Rizvi.

Ni maelezo mafupi ya wasifu wa Mtukufu Mtume wa Mungu mwenye nguvu sana, Muhammad (s.a.w.), ambaye kuhusu yeye Qur'an Tukufu inasema: "*Bila shaka amekufikieni Mtume kutoka miongoni mwenu, yanamhuzunisha yanayokutabisheni, anakuhangaikieni, kwa waumini ni mpole, mwenye kurehemu.*" (9:128)

"*Nasi hatukukutuma ila uwe rehema kwa walimwengu.*" (21:107)

Wakati ambapo jukumu la kuelezea haiba hii kubwa mno ingechukua mijalada mingi, tuna imani kwamba msomaji asiye na upendeleo kwa hakika atanufaika kutokana na toleo hili nyenyekevu.

Tarjuma yake ya Kiswahili inafanywa ipatikane kwa ajili ya faida ya ndugu zetu wazungumzaji wa Kiswahili katika Afrika ya Mashariki na pengine popote.

Tunawashukuru wale wote ambao kwa njia moja au nyingine wamechangia katika utoaji wa tarjuma hii ya Kiswahili ambayo inawasilishwa hapa.

Mchapishaji:
Al-Itrah Foundation
S.L.P. 19701
Dar-es- Salaam, Tanzania.

# MUHAMMAD
# MTUME WA ALLAH

*Kidokezo kifupi cha wasifa*

## Kuzaliwa Mpaka Kuanza kwa Wahyi

Muhammad al-Mustafa, Mtume wa mwisho wa Allah, alizaliwa Makkah, Arabia mnamo mwezi 17 Rabi al-Awaal, mwaka wa kwanza wa tembo (*Amul Fiil*) 570 A.D.

Mtume Muhammad (s.a.w.) alizaliwa katika ukoo wa Bani Hashim, wa kabila la Quraishi, ambao walikuwa ndio walioheshimiwa sana katika familia za Kiarabu. Bani Hashim walikuwa ni kizazi cha Ismail, mwana wa Nabii Ibrahim.

Babu yake Mtukufu Mtume, Mzee Abdul Muttalib alikuwa ndiye Mkuu wa Bani Hashim na vilevile alikuwa ndio mlezi wa al-Kaaba. Baba yake yeye Mtume, alikuwa anaitwa Abdullah na mama yake aliitwa Amina. Baba yake alifariki miezi michache kabla ya kuzaliwa kwake. Akiwa na umri wa miaka sita, Mtume akampoteza mama yake pia na yeye akawekwa chini ya uangalizi wa babu yake, Abdul Muttalib. Lakini babu yake naye akafariki baada ya miaka minne; na safari hii, ami yake Mtume, Abu Talib alichukua dhima juu yake na akawa mlezi wake, akimchukua kuishi naye nyumbani kwake mwenyewe. Hivyo Mtukufu Mtume (s.a.w.) kwa kiasi kikubwa alikulia nyumbani kwa ami yake na hata kabla ya kufikia umri wa balehe alikuwa akifuatana na ami yake kwenye safari za kibiashara kwa misafara.

Mtukufu Mtume hakuenda shule yoyote, hata hivyo, baada ya kufikia umri wa utu uzima alikuwa maarufu kwa hekima zake, hisani, uaminifu na ukweli wake. Mara akawa anajulikana kama "*as-sadiq al-amin* - mkweli, mwaminifu." Ami yake, Abu Talib alikuwa kila mara akisema "Hatujasikia uwongo wowote kutoka kwa Muhammad, wala kuwa

na tabia mbaya au kufanya uharibifu. Kamwe hacheki ovyo ovyo wala kuzungumza wakati usiofaa."

Kwa matokeo ya busara na uaminifu wake, Khadija bint Khuwaylid, bibi wa kikuraishi maarufu kwa utajiri wake, akamteua yeye kama meneja wa biashara zake na akaacha jukumu la kuendesha shughuli zake za kichuuzi mikononi mwake. Mtume safari moja alikwenda Damascus na bidhaa za Khadija na kutokana na uwezo wake akatengeneza faida kubwa ya kuvutia. Haukupita muda mrefu yeye Khadija akamuomba awe mke wake naye Mtume akalikubali ombi lake hilo. Baada ya ndoa yao, akiwa na umri wa miaka ishirini na tano, Mtukufu Mtume akaanza maisha ya kuwa meneja wa mali za mke wake. Alipofikia umri wa miaka arobaini, alijipatia sifa njema ya kuheshimika iliyoenea sana kwa sababu ya busara na uaminifu wake.

Alikataa kuabudu masanamu, kama ilivyokuwa ndio desturi ya kidini ya Waarabu wa wakati huo. Mara kwa mara alifanya faragha za kiroho kwenye pango la Hira nje kidogo ya Makkah, ambamo alifanya maombi na kuzungumza kwa siri na Allah.

## Kuanza kwa Ujumbe

Kwenye umri wa miaka arobaini, wakati Mtume alipokuwa kwenye faragha ya kiroho ndani ya pango la Hira, humo alipokea wahyi wa kwanza kutoka kwa Mwenyezi Mungu s.w.t. kupitia kwa Malaika Mkuu Jibril: Huu ulikuwa ndio mwanzo wa kazi ya kutangaza dini hiyo mpya. Katika muda huo zile aya tano za mwanzo za Sura ya 96 ya Qur'an Tukufu zilishushwa kwake. (Tukio hili linajulikana kama *bi'that* - kusimamishwa ili kutangaza ujumbe wa Allah.)

Siku ile ile aliueleza Wahyi huo kwa binamu yake, Ali Ibn Abi Talib ambaye alitangaza kuikubali kwake dini hiyo. Baada ya Mtume kurudi nyumbani na kumueleza mke wake juu ya Wahyi huo, kadhalika na yeye aliukubali Uislamu. Mara tu, baadaye, Zayd bin Haritha (mtumwa mwaminifu ambaye alimfanya kama mwanawe mwenyewe) vilevile akasilimu na kuwa naye Muislamu.

Mara ya kwanza kabisa wakati Mtukufu Mtume alipokuwa akiwalingania watu kuukubali ujumbe wa Uislamu, alikumbana na upinzai wa kuhuzunisha na mkali sana. Kwa sababu ya umuhimu kwa hiyo, alilazimika kutangaza ujumbe wake kuanzia hapo kwa siri kwa muda wa miaka mitatu hadi yeye alipoagizwa tena naAllah (s.w.t.) kuwaita ndugu zake wa karibu kabisa ili kuukubali ujumbe wake. Aliandaa karamu ya ndugu na akawaalika takriban watu arobaini wa ukoo wake. Katika mkusanyiko huo, Muhammad aliwauliza kama waliwahi kamwe kumuona akidanganya au kusema uongo? Majibu ya jumla yakawa: 'Hatujakuona wewe ukisema uwongo.' Kisha akauliza: "Kama ingekuwa niwaambie kwamba maadui zenu wamejikusanya nyuma ya vile vilima vya mchanga, tayari kwa kuwashambulia, je mtaniamini?" Wao wakajibu, 'Ndio.' Halafu akasema:

> "Simjui mtu yeyote katika Bara Arabu ambaye anaweza kuwapa ndugu zake kitu bora zaidi hasa kuliko ninavyofanya sasa. Mimi ninakupeni furaha ya maisha yote; ya dunia hii na yale ya kesho Akhera. Mwenyezi Mungu ameniagiza mimi kuwaiteni ninyi kwake. Ni nani kwa hiyo, miongoni mwenu atakayenisaidia katika hili, ili awe ni ndugu yangu, mrithi wangu na khalifa wangu?"

Lakini wito huu ulikuwa pia haukuzaa matunda na hakuna aliyeutilia maanani isipokuwa Ali Ibn Abi Talib ambaye kwa hali yoyote ile yeye alikuwa ameikubali dini hiyo. Kwa mujibu wa nyaraka za kumbukumbu za kihistoria na mashairi yaliyotungwa na Abu Talib ambayo yanapatikana hadi sasa, Abu Talib pia aliukubali Uislam; hata hivyo, kwa kuwa alikuwa ndiye mlinzi pekee wa Mtume aliificha imani yake kwa watu ili kuhifadhi ile nguvu yake ya nje aliyokuwa nayo miongoni mwa watu wa Makkah.

Baada ya kipindi hiki, kwa mujibu wa maelekezo ya ki-mungu, Mtume akaanza kulingania ujumbe wake kwa uwazi kabisa. Kwa kuanza kwa kutangazwa kwa wazi kwa ujumbe wake, watu wa Makkah walikuja juu kwa nguvu sana kwa sababu ya ule ujumbe wenyewe wa uislamu - wa kuabudu Mungu mmoja na usawa miongoni mwa waumini bila ya kujali tofauti yoyote ya utaifa, rangi au utajiri - walihofia kabisa dhidi ya hali zao kama zilivyokuwa. Maumivu makali sana na mateso yalifanywa juu ya Mtume na wale walioingia kwenye dini hiyo.

Kwa mfano, Bilal, mtumwa wa kihabeshi ambaye alikuwa ameukubali Uislam, alifungwa kwenye mchanga unaochoma wa jangwa la Arabia na jiwe kubwa sana likawekwa juu ya kifua chake pamoja na maonyo kutoka kwa miliki wake Umayya kwamba angeendelea kubakia katika hali hiyo mpaka atakapoukana Uislam. Lakini sauti pekee ambayo ilisikika ikitoka kwenye midomo  ya Bilal ilikuwa ni "*Ahad! Ahad!*" (Mungu Mmoja! Mungu Mmoja!)

Makuraishi waliwafanyia waumini ukatili sana kiasi kwamba kikundi cha takriban Waislam 100, chini ya uongozi wa Ja'far bin Abi Talib waliziacha nyumba zao na mali zao, na wakahamia Abyssinia (Ethiopia ya sasa). Waliambiwa na Mtume kwamba watamkuta huyo mfalme wa Abyssinia kuwa ni mtawala mwadilifu. Wakiwa na nia ya kukwamisha kule kuenea kwa Uislamu, Makuraishi waliwafuata mpaka huko Abyssinia wakitafuta kurejeshwa kwao nyumbani ili waje kuhukumiwa kama wahalifu. Lakini Ja'far, kwa ufasaha sana aliliwasilisha suala la Waislam kwa mfalme wa Abyssinia na maombi ya Makuraishi yakakataliwa. Ja'far akasema:

> "Ewe Mfalme! Sisi tulikuwa tumezama kwenye kina cha ujahiliya na ushenzi; tuliabudu masanamu, tuliishi maisha machafu tulikula mizoga na tulizungumza lugha ya machukizo; tuliipuuza kila hisia ya ubinadamu na shughuli zote za ukarimu na ujirani; tulikuwa hatuna wala hatujui sheria yoyote bali ile ya wenye nguvu - wakati Mwenyezi Mungu alipotunyanyulia mtu miongoni mwetu, ambaye uzao wake mtukufu, ukweli wake, uaminifu na usafi wake, vyote tunavitambua; na ametuita kwenye Upweke wa Allah (Tawheed) na akatufundisha tusimshirikishe Yeye na kitu chochote; ametukataza tusiabudu masanamu; alituagiza sisi tuseme kweli, kuwa waaminifu kwenye amana zetu, kuwa wenye huruma na kuwajali haki za majirani; ametukataza tusiwaongelee wanawake kwa uovu au kula mali ya mayatima; alituagiza kuepukana na tabia mbaya na kujizuia na maovu; tusali, tutoe zakat na kufunga.
>
> Tumemwamini yeye, tumeyakubali mafundisho yake na amri zake za kumuabudu Mungu na tusishirikishe chochote pamoja Naye.
>
> Kwa sababu hii tu, watu wetu wamechachamaa dhidi yetu,

wametutesa ili tuachane na ibada ya Mungu na turudi kwenye kuabudu masanamu ya mawe na magogo ya miti na machukizo mengineyo. Walitutesa na kutuumiza, mpaka tukawa tumekosa usalama tukiwa miongoni mwao, tumekuja kwenye nchi yako nasi tunategemea kwamba utatulinda kutokana na uonevu wao."

Nyuma, huko Makkah, vikwazo vya kiuchumi na kijamii viliwekwa dhidi ya Mtume na familia yake. Kwa hiyo, Mtume na ami yake, Abu Talib, pamoja na ndugu zao kutoka ukoo wa Bani Hashim walikimbilia kujihifadhi mafichoni kwa muda wa miaka mitatu huko kwenye "korongo la njia ya mlimani" - lililoitwa 'Shi'b Abu Talib' ngome moja iliyokuwa kwenye moja ya mabonde ya Makkah. Hakuna aliyefanya uhusiano au kushughulika nao na wala wao hawakuthubutu kuiondoka hiyo sehemu yao ya hifadhi.

Ingawa hapo mwanzoni waabudu masanamu wa Makkah walifikiria kuwafanyia aina zote za mashinikizo na mateso kama vile kuwachapa na kuwapiga, kuwatukana, dhihaka na kashfa kwa Mtume, mara kwa mara wao walionyesha upole pia na hisani kwake ili kuweza kumfanya aiwache kazi ile ya ujumbe wake. Waliweza kumuahidi viwango vikubwa vya fedha au uongozi na utawala wa kikabila. Lakini kwa Mtume, ahadi zao za na vitisho vyao viliishia tu katika uongezekaji wa nia na dhamira yake ya kuitekeleza kazi ya ujumbe wake. Wakati mmoja, wao walipokuja kwa Mtume wakimuahidi utajiri na mamlaka, Mtume, akitumia lugha ya kiistiari aliwaambia, kwamba kama ingekuwa waliweke jua kwenye kiganja cha mkono wake wa kulia na mwezi kwenye kiganja cha mkono wa kushoto, yeye asingegeuka nyuma katika kumtii Mungu Mmoja ama kujiepusha na kufanya kazi ya ujumbe wake.

## Kuhama Kwanda Makkah

Katika takriban mwaka wa kumi wa Utume wake, wakati Mtume alipoondoka kwenye "bonde la Shi'b Abu Talib", ami yake, Abu Talib, ambaye pia alikuwa ndiye mlinzi wake pekee, alifariki dunia, kama alivyofariki pia mke wake mpendwa Khadijah. Kuanzia hapo ikawa hakuna tena ulinzi wa maisha yake wala mahali pa kukimbilia.

Hatimaye wale waabudu masanamu wa Makkah walibuni mpango wa siri wa kumuua Mtume. Wakati wa usiku wao waliizunguka nyumba yake kwa nia ya kuivamia nyumba yake mwishoni mwa usiku na kumkata kata vipande vipande wakati akiwa kitandani. Lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu alimjulisha kuhusu mpango huo na kamuamuru kuondoka na kwenda Madina, wakati huo ikiitwa Yathrib. Mtume alimwambia Ali alale kitandani mwake ili kwamba maadui wasigundue kutokuwepo kwake; bila kusita Ali alikubali kutoa mhanga maisha yake kwa ajili ya Mtume na akalala katika kitanda cha Mtume. Kisha Mtume akaondoka hapo nyumbani chini ya ulinzi Mtukufu wa kimbinguni, akiwapita maadui zake katikati yao, na akichukua hifadhi ndani ya pango karibu na Makkah. Baada ya siku tatu, maadui zake, baada ya kutafuta kila mahali, walikata tama ya kumkamata yeye na wakarudi Makkah. Mtume naye akaondoka kuelekea Yathrib.

## Kuanzisha Jamii ya Kiislamu

Watu wa Yathrib, ambao uongozi wao walikuwa tayari walikuwa wamekwisha ukubali ujumbe wake Mtukufu Mtume na kula kiapo cha utii kwake, walimkaribisha kwa ukarimu kabisa na wakayaweka maisha na mali zao chini ya mamlaka yake. Huko Yathrib, kwa mara ya kwanza, Mtume aliunda Jumuiya ndogo ya Kiislam na akawekeana saini mikataba na makabila ya Kiyahudi, ndani na kandoni mwa mji huo, vilevile na yale makabila ya kiarabu yenye nguvu katika eneo hilo. Alijiandaa kuyafanya kazi ya kuutangaza ujumbe wa Uislam na Madina ikawa maarufu kama "Madinatu 'r-Rasul" (Mji wa Mtume). Baadae kabisa ulikuja kujulikana kama "Madina".

Uislam ulianza kukua na kupanuka kuanzia siku hadi siku. Wale Waislamu, ambao huko Makkah walikuwa wamenasa kwenye nyavu za uonevu na dhulma za Makuraishi, pole pole waliyaacha majumba na mali zao na wakahama kwenda Madina, wakimzunguka Mtume kama wadudu nondo waliozunguka mshumaa. Kundi hilo lilijulikana kama "wahamiaji" (*Muhajiriin*) kwa namna ile ambayo wale waliomsaidia Mtume huko Yathrib walivyojipatia jina la "Wasaidizi" (*Ansar*).

Mtume aliinda jamii hiyo katika misingi ya haki na usawa miongoni mwa waumini. Undugu - sio tu kwa maneno bali pia kwa vitendo - ulianzishwa miongoni mwa Muhajir na Ansar. Mfumo wa kijamii wa Kiislam uliweza kupanua uadilifu na ulinzi wake hata kwa wasiokuwa Waislam chini ya utawala wake.

## Mapambano Katika Medani za Vita

Uislam ulikuwa unaendelea haraka sana lakini wakati huo huo wale waabudu masanamu wa Makkah, na vilevile makabila ya Kiyahudi ya Uarabuni, yalikuwa hayazuiliki katika kuwabughudhi kwao Waislamu. Kwa msaada wa wanafiki wa Madina, ambao walikuwa miongoni mwa jamii ya Waislam, walisababisha mabalaa mapya kwa ajili ya Waislam kila uchao hadi mwishowe jambo hilo likaongezea kwenye vita.

Vita vingi vilitokea kati ya Waislam, washirikina wa Kiarabu na Wayahudi. Waislam waliibuka washindi katika mengi ya mapambano hayo. Katika mapigano yote makubwa kama vile vita vya Badr, Uhud, Khandaq, Khaybar, Hunayn na kadhalika, Mtume alikuwepo mwenyewe katika uwanja wa mapambano. Vilevile katika vita vyote vikubwa na vidogo vingi, ushindi ulipatikana zaidi kwa kupitia juhudi za Ali bin Abi Talib. Alikuwa ndiye mtu pekee ambaye kamwe hakugeuka kwenye vita vyovyote kati ya hivi. Katika vita vyote vilivyotokea katika miaka kumi yote baada ya kuhama kutoka Makkah kwenda Madina, chini ya Waislamu miambili, na makafiri chini ya elfu moja waliuawa.

***(a) Vita vya Badr:***

Watu wa Makkah waliendeleza majaribio yao ya kuuvunja Uislamu. Waliendelea kuwabughudhi Waislam waliokuwa wamebakia hapo Makkah na pia walikamata mali na vitu vyao. Abu Jahl, kiongozi wa watu wa Makkah, alituma hata barua kwa Mtume akimtishia na shambulio kutoka kwa watu wa Makkah. Ilikuwa ni katika kujibu uchochezi huu ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu alimpa Mtume ruhusa ya kuwapiga makafiri wa Makkah. Yeye alisema:

> "*Imeruhusiwa (kupigana) kwa wale wanaopigwa, kwa sababu wamedhulumiwa... Ambao wametolewa majumbani mwao pasipo haki.....*" (22:39-40)

Katika mwaka wa **pili** wa Hijiria, Mtume akiwa na takriban Waislamu 300 wasioandaliwa vizuri, walikabiliana na jeshi lililoandaliwa vema kutoka Makkah lenye takriban wapiganaji 1,000. Ingawa walizidiwa kwa idadi, Waislam waliweza kuwashinda makafiri katika pambano la kwanza la silaha dhidi ya maadui.

***(b) Vita vya Uhud:***

Ili kulipiza kisasi cha kushindwa kwao huko Badr, watu wa Makkah waliandaa kikosi kingine cha jeshi katika mwaka wa **tatu** wa hijiria na wakatoka kuelekea Madina. Baada ya kuvifikia vilima vya Uhud, maili nne nje ya madina, Mtume alichukua nafasi yake chini ya mlima. Jeshi likajipanga katika mifumo ya mapigano. Watupa mishale 50 waliwekwa chini ya kamandi ya Abdullah bin Jubair kwenye kijinjia katikati ya vilima hivyo ili kuwalinda Waislamu na mashambulizi yoyote kutoka upande wa nyuma. Walikuwa na maagizo makali ya kutokuondoka kwenye sehemu zao, kwa matokeo yoyote ya vita yatakayokuwa.

Waislamu mwanzoni waliwashinda watu wa Makkah. Maadui hao, baada ya kushindwa na kupata hasara kubwa, walirudi nyuma kwa mparaganyiko na Waislam wakaanza kukusanya ngawira.

Wakidhania kwamba mapigano yamekwisha; wengi wa wale watupa mishale 50 wanaochunga vile vilima waliondoka kwenye sehemu zao kinyume na amri ya kiongozi wao. Khalid bin Walid, kamanda mmoja wa kikosi cha farasi cha jeshi la Makkah aliikamata fursa hii na akakiongoza kikosi chake kupitia kwenye kinjia hicho cha mlimani na baada ya kuwauwa wale watupa mishale wachache waliokuwa wamebakia, alianzisha shambulizi kali juu ya Waislam kutoka upande ule wa nyuma.

Kwa sababu ya kuasi na kutotii amri kwa kikundi kidogo, ule ushindi wa Waislamu ukachukuliwa kutoka mikononi mwao Waislam. Wengi wao wakakimbia kutoka kwenye uwanja wa mapambano. Wachache tu, hususan Ali, walisimama imara na kupigana mpaka mwisho. Hatimae Waislamu wakakimbilia kwenye usalama wa vilele vya mlima wa Uhud. Miongoni mwa wale Waislam 70 ambao walikufa katika shambulizi hili la majibu la watu wa Makkah alikuwa ni Hamza bin Abdul Muttalib, yule

ami yake jasiri Mtume. Yeye kwa hakika alikuwa ni simba wa Mungu (*Assadullah*).

***(c) Vita vya Khandaq (Ahzab):***

Katika mwaka wa **tano** hijiria, kabila moja la kiyahudi liliunda ushirikiano na watu wa Makkah; na kwa pamoja wakaandaa jeshi la takriban wapiganaji 10,000. Vita hivi vinajulikana kama vita vya *Ahzab* (ushirikiano) na vilevile *Khandaq* (Mtaro, handaki) kwa sababu Waislamu walichimba mitaro kuzunguka kambi yao ili kumzuia adui kuingia mjini.

Yale majeshi ya muungano ya wasiokuwa Waislamu yaliizingira Madina kwa mwezi mmoja. Isipokuwa kwa wapiganaji mashuhuri wachache tu, walikuwa hawana uwezo wa kuvuka ule mtaro. Majeshi hayo ya muungano mwishowe yalirudi nyuma baada ya Ali, katika pambano la mtu mmoja mmoja, alipomuua yule jasiri kabisa wa hao wapiganaji wao.

***(d) Vita vya Bani Qurazah:***

Hawa Bani Qurazah walikuwa wamefikia makubaliano ya mkataba na Waislam, lakini waliukiuka mkataba huo kwa kujiunga na watu wa Makkah katika vita vya *Ahzab*. Hivyo, baada ya vita vya *Ahzab*, Waislamu walisonga mbele kuwaendea Bani Qurazah ambao mwishowe walisalimu amri kwa Waislamu. Mtume alipendekeza kwao wao kukubali usuluhishi wa Sa'd bin Ma'z. Wao walikubali na wakashughulikiwa kwa uamuzi wake: kuwauwa wapiganaji na kutaifisha mali zao.

***(e) Vita vya Bani Mustalaq:***

Katika mwaka wa **sita** wa hijiria, lile kabila la Mustalaq lilikiuka haki za Waislam. Na matokeo yake, iliwabidi wakabiliane na majeshi ya Waislam mahali panapoitwa Maris'a na walishindwa vita hivyo.

***(f) Vita vya Khaybar:***

Idadi kubwa ya makabila ya kiyahudi yalifanya makazi yao katika ngome za khaybar na maeneo ya karibuni ya Arabia ya kaskazini. Walikuwa na ushirikiano wa karibu sana na watu wa Makkah na walikuwa kila mara wakiwatishia Waislam. Katika mwaka wa **saba** wa hijiria, Mtume aliamua

kumkabili adui. Waislamu walitoka kijeshi kwenda Khaybar, wakaizingira na hatimae wakapata ushindi baada ya Ali kusonga mbele, akaiteka ile ngome kuu na akamuua yule shujaa jasiri mkuu kuliko wapiganaji wote wa Kiyahudi.

## Mkataba wa Hudaybia & Kuanguka kwa Makkah

Katika mwaka wa **sita** wa hijiria, Mtume aliamua kwenda Makkah kuhiji. Watu wa Makkah waliwazuia Waislamu mahali panapoitwa Hudaybia na hawakuwaruhusu kuingia mjini hapo. Makabiliano haya yaliishia kwenye mkataba wa amani baina ya Mtume na Makuraishi wa Makkah. Mkataba huu wa amani ulijenga mazingira salama kwa kiasi fulani kwa Mtume kuanza kupanua ule wito wa Uislamu kwa makabila na watu walio mbali na bara Arabu.

Kama matokeo ya shughuli za Mtume na jitihada zisizo na ubinafsi za Waislam katika kipindi kile, Uislam uliendea kote katika peninsula ya Arabia. Zilikuwepo pia barua zilizoandikwa kwa wafalme wa nchi zingine kama vile Uajemi, Byzantine na Abyssinia zikiwaalika wafalme hao kuukubali Uislamu.

Wakati huu Mtume aliishi katika umasikini na ufukara na alikuwa na fahari nayo hali hiyo. Hakuwahi kutumia muda wake wowote bure bure tu. Bali muda wake wote uligawanywa katika sehemu tatu: moja kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, katika kumuabudu na kumkumbuka Yeye; sehemu nyingine kwa ajili yake binafsi na watu wa nyumbani kwake na mahitaji ya nyumbani; na sehemu kwa ajili ya watu. Katika wakati wa sehemu hii ya muda wake alijishughulisha katika kueneza na kufundisha Uislamu na elimu zake, kusimamia mahitaji ya jamii ya Kiislamu, kuondoa maovu yoyote yaliyokuwepo, kuhudumia mahitaji ya Waislam, kuimarisha mafungamano ya ndani na nje, na mambo mengine kama hayo.

Moja ya masharti ya mkataba huu wa amani lilikuwa ni kwamba Maquraishi wasingeweza kuwadhuru Waislamu au yoyote kati ya washirika wao walioungana nao. Sharti hili, hata hivyo lilikiukwa na Maquraishi pale walipolisaidia kabila la Bani Bakr dhidi ya kabila la Bani

Khuza'a - hilo la kwanza ni washirika wa Maquraishi na hili jingine ni washirika wa Waislamu. Mtume aliwaomba Maquraishi kuheshimu mkataba huo, wavunje ushirikiano wao na kabila la Bani Bakr na kuwafidia wale waathirika wa uchokozi wao. Maquraishi walikataa kutii na kufuata masharti ya mkataba wao. Mtume, akiwa na jeshi lililoandaliwa vizuri lenye nidhamu ya hali ya juu, lenye takriban askari 10,000 liliingia Makkah katika mwaka wa **nane** baada ya hijiria na wakaiteka bila upinzani mkubwa.

Mji huo, ambao ulikuwa umekataa ujumbe wake, na kupanga njama dhidi ya wafuasi wake na wakaungana katika njama ya kumuua yeye, sasa akawa chini ya huruma yake. Mtume aliwauliza watu wa Makkah: "Ni nini mnachoweza kutarajia kutoka kwangu?" Wao wakajibu: "Huruma! Ewe bwana mkarimu na mtukufu!" Kama angependa, angeweza kuwafanya wote kuwa watumwa wake. Lakini Muhammad - "rehma kwa ajili ya ulimwengu" - akasema: "Nitaongea nanyi kama Yusuf alivyoongea na ndugu zake. Sitawasuteni leo; Mwenyezi Mungu atakusameheni, kwani Yeye ni Mwingi wa Huruma na Upendo. Nendeni, mko huru kabisa!"

Kwa kuanguka kwa Makkah, kila kizuizi cha mwisho katika njia ya Uislamu kilikuwa kimeondolewa na watu wengi na makabila ya Waarabu katika peninsula ya Arabia yakaanza kuukubali ujumbe wa Uislam. Hivyo ule mwaka wa **tisa** wa hijiria unajulikana kama "Mwaka wa ujumbe" kwa sababu ya ile idadi ambayo siyo ya kawaida ya wajumbe waliokuwa wakija Madina kuja kutoa heshima zao kwa Mtume hapo Madina.

## Hijja ya Mwisho & Kifo

Katika mwaka wa **kumi** wa hijiria, Mtume aliamua kwenda kufanya Hijja. Aliwaalika Waislamu kuungana naye na wajizoeshe kanuni za hija. Zaidi ya Waislam laki moja waliungana naye katika hijja hii. Ingawa hii ni hijja ya mwanzo na ya mwisho ya Mtume, lakini inajulikana kama "*al-Hajjatu 'l-wida'* — Hija ya Muago." Aliichukua fursa hii ya ule mkusanyiko ambao haujawahi kutokea ili kuwakumbusha Waislamu juu ya mambo mengi muhimu na thamani ya Uislam.

Akiwa njiani akirudi kwenda Madina, alisimama mahali panapoitwa Ghadir Khum na akatoa hotuba ndefu sana ambamo alifanya muhtasari wa yale mafundisho muhimu makuu ya Uislam, akawajulisha kuhusu kifo chake kilichokuwa kina karibia na akamteua Ali bin Abi Talib kuwa mrithi wake.

Baada kuishi kwa miaka kumi ya Madina, Mtume aliugua na kufariki baada ya siku chache tu za maradhi yake. Kwa mujibu wa Riwaya zilizopo, maneno ya mwisho kwenye midomo yake yalikuwa ni ushauri kuhusiana na watumwa na wanawake.

## Heshima ya La Martine kwa Mtume

Mwanahistoria wa kifaransa wa karne ya kumi na nane, La Martine, anaandika yafuatayo katika kitabu chake *Histoire de la Turquie* (1854) kuhusu Mtume wa Uislam:

> "Kamwe mwanadamu hajajiwekea mwenyewe, kwa hiari au bila kukusudia, lengo adhimu sana, kwa lengo hili lilikuwa la nje ya uwezo wa kibinadamu: Kuangamiza imani za ushirikina ambazo zilikuwa zimeingilia kati baina ya mwanadamu na muumba wake, kumrudisha Mungu kwa mwanadamu na mwanadamu kwa Mungu; kudumisha lile wazo la kimantiki na tukufu la kimungu katikati ya vurugu za miungu ya kidunia na yenye sura mbaya ya uabudu masanamu uliokuwepo wakati huo...
>
> "Kama ukuu wa lengo, ufinyu wa nyenzo, na matokeo ya kushangaza ndivyo kigezo halisi cha kipaji cha kibinadamu, ni nani angeweza kuthubutu kumlinganisha mtu yoyote maarufu katika historia ya kisasa na Muhammad?...
>
> "Mwanafalsafa, msemaji mwenye fasaha, nabii, mwanasheria, mpiganaji, mtekaji wa mawazo, mdumishaji wa imani zenye mantiki, mtindo usiokuwa na sura mbali mbali (makundi); mwanzilishi wa dola ishirini za kidunia na ufalme mmoja wa kiroho, huyo ni Muhammad. Na kuhusu vipimo vyote ambavyo kwavyo umaarufu wa kibinadamu unaweza kupimwa navyo, tunaweza kuuliza, hivi kuna binadamu yoyote mashuhuri kuliko yeye?"

***

Kidokezo hiki kifupi cha wasifa wa Mtukufu Mtume
kinatoka kwenye kitabu kiitwacho:
***Islam: Faith, Practice & History.***

Vitabu vinavyopendekezwa juu ya maisha ya Mtume

1. *A Glance at the Life of the Prophet of Islam*
   By Dar Rah-e Haq, Qum.

2. *The Life of Muhammad the Prophet*
   By Syed Saeed Akthar Rizvi

3. *The Message*
   By Ja'far Subhani

4. *Muhammad: A Western Attempt to Understand Islam*
   By Karen Armstrong

Vitabu 1 hadi 3 vinapatikana katika tovuti la www.shia-maktab.info

**Mfululizo wa vitabu juu ya:**
***Mtu Mwenye Athari Kubwa Sana Katika Historia***

1. Muhammad Mtume wa God.
2. Amani & Jihadi katika Uislam.
3. Uislam ulieneaje? Kwa upanga au kwa mazungumzo.
4. Mitala & Ndoa za Mtume.
5. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad.

*"Uchaguzi wangu wa Muhammad kuongoza orodha ya watu wenye ushawishi na umaarufu zaidi katika dunia unaweza ukawashangaza baadhi ya wasomaji na unaweza ukahojiwa na wengine, lakini yeye alikuwa ndiyo mtu pekee katika historia ambaye alikuwa amefanikiwa sana mno katika kiwango cha kidini na kidunia pia."*

*Michael H. Hart*
*The 100 Most Influential Persons in History*

*"... (Yeye) alikuwa Kaisari na Papa kwa pamoja; hali alikuwa ni Papa bila vile visingizio vya Upapa, na Kaisari bila vile vikosi vya askari vya Kaisari. Bila jeshi la kudumu, bila mlinzi binafsi, bila jumba la utawala - IKULU -, bila mapato yaliyotengwa endapo kamwe mtu yoyote alikuwa na haki ya kusema kuwa alitawala kwa haki ya Ki-Mungu, alikuwa ni Muhammad; kwani alikuwa na mamlaka na madaraka yote bila ya vyomho vyake na bila ya misaada yake."*

*Rev. Bosworth Smith*
*Mohammed & Mohammedanism (1874)*

*Kimetolewa na*

**Al-Maʿārif Publications**
Toronto, Canada

www.al-m.ca | publications@al-m.ca | (+1-416) 624-7861